

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA TATU

YATOKANAYO NA KIKAO CHA HAMSINI NA NNE

30 JUNI, 2016

MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA HAMSINI NA NNE

TAREHE 30 JUNI, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt.Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

Mara baada ya Dua kusomwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walitoka nje ya Ukumbi wa Bunge.

Makatibu Mezani Awamu ya Kwanza:

1. Ndg. Ramadhan Ruhilabake
2. Ndg. Ramadhani Abdallah
3. Ndg. Thomas D. Kasililla – KB
4. Ndg. John J. Joel – NKB
5. Ndg. Nenele Mwiambi – MSB

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

- i) Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) aliwasilisha Mezani Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2015 (*The Annual Report and Audited Accounts of the National Environment Management Council (NEMC) For the Year Ended 30th June, 2015*).
- ii) Mhe. Ashatu Kijaji Kachwamba, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Mezani Taarifa ya Mwaka ya Mfuko wa PPF kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2015 (*The Annual Report of PPF Pensions Fund for The Year Ended 30th June, 2015*).
- iii) Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi aliwasilisha Taarifa ya Shughuli za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Mwaka 2014/2015 (*Report of the Activities of the Open University of Tanzania for the Year 2014/2015*).
- iv) Mhe. George Huruma Mkuchika, Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge aliwasilisha Taarifa ya Kamati hiyo kuhusu Shauri la Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi (Mb) kuhusiana na kutoa Ishara ya matusi Bungeni.

III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge:-

OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na.461 - Mhe. Venance Mwamoto [kny. Mhe. Khatib Said Haji]

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Venance Mwamoto
(ii) Mhe. Faida Mohammed Bakari
(iii) Mhe. Abdallah Hamisi Ulega

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na.462 - Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula [kny. Mhe. Mariam Nassor Kisangi]

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula
(ii) Mhe. Ally Keissy Mohammed
(iii) Mhe. Sikuchan Yassin Chikambo
(iv) Mhe. Zakaria Paulo Issaay

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na.463 Mhe. Deogratias Francis Narawa

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Deogratias Francis Ngalawa
(ii) Mhe. Suleimani Muradi Sadiq
(iii) Mhe. Ignas Aloyce Malocha
(iv) Mhe. Hamida Mohammed Abdallah

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Swali Na.464 – Mhe. Jamal Kassim Alli

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Jamal Kassim Alli
(ii) Mhe. Seif Said Gulamali
(iii) Mhe. Salum Mwinyi Rehani
(iv) Mhe. Joram Ismail Hongoli

Swali Na.465 – Mhe. Issa Ali Mangungu [kny. Mhe. Lucy Simon Magereli]

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Issa Ali Mangungu
(ii) Mhe. Richard Mganga Ndassa
(iii) Mhe. Hussein Mohammed Bashe

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Swali Na.466 – Mhe. Amina Nassoro Makilagi

- Swali la nyongeza: Mhe. Amina Nassoro Makilagi

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na.467 – Mhe. Augustino Manyanda Masele

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Augustino Manyanda Masele
(ii) Mhe. Flatei Gregory Massay
(iii) Mhe. Desderius John Mipata
(iv) Mhe. Dotto Mashaka Biteko

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na.468 – Mhe. Goodluck Asaph Mlinga [kny. Mhe. Marwa Ryoba Chacha]

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Goodluck Asaph Mlinga
(ii) Mhe. Kangi Alphaxard Lugola
(iii) Mhe. Angelina Adam Malembeka

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na.469 – Mhe. Mendrad Lutengano Kigola

- Swali la nyongeza: (i) Mhe. Mendrad Lutendano Kigola
(ii) Mhe. Rose Cprian Tweve
(iii) Mhe. Shaaban Omary Shekilindi

IV. MATANGAZO:

- i) Matangazo mbalimbali ya Wageni waliofika Bungeni yalitolewa.
- ii) Matangazo mbalimbali ya vikao vya kazi yalitolewa.

V. KAULI ZA MAWAZIRI:

- i) Waziri wa Katiba na Sheria alitoa Kauli kuhusu kesi ya Jinai namba 100 ya Mwaka 2016 ya Jamhuri dhidi ya Isaac Habakuk Emily iliyoamuliwa na Mahakama ya Hakim Mkaazi Arusha;
- ii) Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alitoa Kauli kuhusu tukio la ujambazi lililotokea Jimboni Rufiji tarehe 28/6/2016.

VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Miswada ifuatayo ilisomwa kwa mara ya kwanza:-

- i) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2016 (The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016).
- ii) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, wa Mwaka 2016 (The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016).

VII. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mhe. George Huruma Mkuchika alitoa Hoja ya Kamati hiyo kuhusu Shauri la Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi kutoa ishara ya matusi Bungeni.

Hoja hiyo ya Kamati ilihitimishwa kwa Bunge kumpa adhabu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi asihudhurie vikao kumi vya Bunge kuanzia kikao cha tarehe 30/6/2016.

VIII. MIONGOZO WA SPIKA:

Naibu Spika alitoa majibu ya miongozo mbalimbali iliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge.

IX. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

Katibu wa Bunge alitoa Taarifa ya kukamilika rasmi kwa Shughuli za Bunge zilizopangwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge.

X. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa alitwa kutoa Hotuba yake ya kuliahirisha Bunge, ambapo Bunge liliahirishwa hadi tarehe 6/9/2016 Siku ya Jumanne, saa 3.00 kamili asubuhi katika ukumbi wa Bunge Mjini Dodoma.

XI. MATANGAZO YA ZIADA:

- i) Naibu Spika aliwatambulisha Wageni mbalimbali ambao hawakutangazwa asubuhi.
- ii) Naibu Spika aliwatambua Watumishi wawili wa Bunge wanaostaafu Utumishi wa Umma siku hiyo ambao ni Ndg. John N. Joel [NKB(B)] na Ndg. Abdallah Suleiman(Mhudumu)

XII. TAARIFA YA SPIKA:

Spika alitoa Taarifa kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea kwenye Mradi wa Utambuzi wa Mfumo wa Alama za Vidole (AFIS) unaotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao unafuatiliwa na Kamati ya Bunge ya PAC kutokana na Taarifa iliyotokana na Taarifa ya CAG.

XIII. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 7.35 mchana Mheshimiwa Naibu Spika aliahirisha Bunge hadi tarehe 06 Septemba, 2016 baada ya kuimbwa wimbo wa Taifa

**DODOMA
30 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**